Msururu wa Upotofu na Udanganyifu




# We Kafiri!

Janga la kuwakufurisha Waislamu kwa Makosa ya kisharia

Muislamu kumwambia Muislamu “ We Kafiri! ”

Toleo

2

SANAD

Sw

بسم الله الرحمن الرحيم

Kila jinsi ya sifa njema ni za Allah Mlezi wa viumbe wote,
Rehma na Amani zimshukie mbora wa Manabii na Wajumbe,
Nabii wetu Bwana Muhammad na Jamaa zake na Swahaba zake wote.

# JANGA GENI:KUPOTOKA FIKRA

Limeenea katika zama hizi zama mwisho naina ya Waislamu janga la kukufurisha, na wamelifanya sahali watu wengi jambo hilo hadi imekua kuskia ibara " We Kafiri " ni jambo la kawaida kwa watu, na hilo limesababisha kuenea Fitna na kutojali Umwagaji damu walaa kuvunjiana hishma na kuwaasi wazazi na kukata vizazi, ikawa wapigana kwa kisingizio cha wajibu wa kurekibisha itikadi mwanzo, na hilo si kwa lengine ila ni kwa sababu ya kutosoma dini na upungufu wa kujua Uislamu swahihi.

S ; Je yafaa Muislamu kumuambia Muislamu " We Kafiri " ?



## Halifai hilo

kwa neno la Mtumi Rehma na Amani ziwe juu yake na jamaa zake.
(Mtu yoyote atakae mwambia ndugu yake : "We Kafiri" basi litamwangukia mmoja wao, [alieitwa] ikiwa ni kweli ama litamrudia mwenyewe).[1]

Na kwa neno lake Rehma na Amani ziwe juu yake katika alilopokea Abu Dhar R.A. :
(Na atakae muita mtu Kafiri ama akasema "We Adui wa Allah" wala sio hivo ila litamrudia yeye)[2] Na maana litamrudia yani utamrudia yeye Ukafiri.

Na kwa neno lake Rehma na Amani ziwe juu yake na Jamaa zake, katika aliolopokea Abu Said Al-Khudriy :
(Hamkufurishi mtu mwenzake kinamna yoyote ila hubakia nalo mmoja wao ikiwa ni Kafiri la sivo atakua Kafiri kwa kumkufurisha).[3]

(1) Imepokelewa na Bukhari na Muslim .

(2) Imepokelewa na Bukhari na Muslim .

(3) Imepokelewa na Ibnu Habaan katika Swahihi yake mlango wa Imani .

# KUFIKIRIA KIMAKOSA - KUFAHAMU KIMAKOSA

Lakini katika Waislamu si kunao wanaokufurishwa kwa matendo yao?



Kila anaeshuhudia kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki illa ni Allah na kwamba Muhammad ni Mtumilizwa na Allah na akafurahishwa na mema na akachukizwa na mabaya basi [huyo] ni mu'min.

Kutoka kwa Kiongozi wa waumini Umar bin Khatwaab R.A. amesema Mjumbe wa Allah S.A.W. amesema : (Atakaefurahishwa na mema yake na akachukizwa na mabayayake, basi huyo ni Mu'min) ; "hivo laiti nijue anaemwambia Ndugu yake: "We Kafiri" nayeye ni katika wanao furahishwa na mema yake na kuchukizwa na mabaya yake, ni kwa nini kumtolea ushahidi Ukafiri kuliko kumshuhudia Imani?"(1)

Na katika Hadithi ya A'amash kutoka kwa Abi Sufyaan, alisema: nilimwambia Jabir R.A. : "Je mulikua mukimwambia yoyote kati ya wanaolekea Qibla [neno] Kafiri? akasema: hapana , nikamwambia: Je Mushrik? akasema Allah anilinde ; na akaondoka"(2)

Lakini Allah Alietukuka amesema: ( Na ambae hatahukumu kwa aliyoyateremsha Allah basi hao ndio Makafiri). kwa hio wasmamizi wote ambao hawatekelezi Sharia ni Makafiri, na pia kila alieridhia usmamizi wao katika raia, je si hivo?

Sivo , hivo sio sawa sababu Maswahaba na Waliowafuatia na Wanavyuoni wengi wamefasiri maana ya Ukafiri hapa kua ni Ukafiri chini ya Ukafiri , yani ni makosa makubwa, lakini hayamtoi anaeyafanya ndani mwa Uislamu.

Nani aliosema ni Ukafiri chini ya Ukafiri?



Amesema hilo Ibnu Abbaas na Hudheifa na Twauus na Mujahid na Ahmad bin Hanbal na Ibnu Abdil-Bar na Wafasiri wengi kama IbnuJurair na Fakhrur-Raziy na Al-Baghawiy na Al-Khaazin na Al-Qurtubiy na wengineo.(3)

Na vp wanashikilia sana baadhi ya Mashekhe na Wahubiri kwamba wale ambao hawahukumu kwa aliyoyateremsha Allah, ni Makafir?

Mwenye kushikilia hilo basi yeye anajengea kwa hilo itikadi ya Khawarij wala sio itikadi ya Ahlu sunna.

Amesema Imaam Al-Qurtubiy katika [kitabu] Al-mufhim: " Na neno lake [Allah] Alietukuka: ﴿Na ambae hatahukumu kwa aliyoyateremshaAllah, basi hao ndio Makafiri﴾ . wanasimamisha hoja kwa maana yake ya nje Wanaokufurisha [watu] kwa madhambi nao ni Makhawarij, wala hawana hoja ndani yake.(4)

Na amesema Imaam Samaaniy katika tafsiri yake: " Na ujue kua Khawarij wanatolea dalili aya hini kua asiehukumu kwa aliyoyateremsha Allah huyo ni kafiri, na Ahlu Sunna wamesema hawi Kafiri kwa kuacha kuhukumu [kwa aliyoyateremsha Allah]". (5)

(1) Ibnu Abdil-Bar katika [Kitabu] At-Tamhiid fi Al-Muwatwa'a (17/15-22)

(2) Kitabu kilichotangulia, na imepokelewa na Abu Yaalaa na At-Twabraniy, na wapokezi wake ni Swahihi kama alivoileta Al-Haiytamiy kwenye Majmauz-Zawaid.

(3) imetajwa kwa upana kwenye kijitabu cha kwanza.

(4) Al-Mufhim lima Ashkala min Talkhiswi Muslim cha Abil-Abbaas Al-Qurtubiy 2/116

(5) Tafsiri ya Imaam As-Samaaniy 2/42

# DHANA NA PUZUKO ZA BAADHI YA WAHUBIRI



**Je katika Waislamu kuna anaomshirikisha Allah shirki kubwa inayomtowa kwenye Uislamu?**

Hapana kati ya Waislamu anaemshirikisha Allah shirki kubwa inayomtowa kwenye Uislamu.

**Ni ipi dalili ya hayo?**

Dalili ya hilo ni neno la Mtumi Rehma na Amani ziwe juu yake alilopokea Uqba bin Aamir R.A. : (Wallahi mimi siwaogopei mufanye shirki baada yangu, lakini nawaogopea mushindanie ndani yake [Dunia]).[1]

**Wanazoni wamefahamu nini kutokana na haya maneno ya Mtumi?**

Wamethibitisha nayo kukhofia Umma kushindania Dunia itakayowapelekea kwenye maangamivu yao, na wakaondoa nayo khofu yoyote juu ya Umma kutokana na shirki kubwa, kama alivoeleza Mtumi Rehma na Amani ziwe juu yake na Jamaa zake. na miongoni mwao neno la Imaam Ibnu Abdul-Bar katika [Kitabu] Al-Tamhiid:

" **Na atakae khofia Umma wa [Nabii] Muhammad kitu ambacho hakukikhofia mwenyewe, atakua amepondoka kwa namna isiofichika**".[2]



**Lakini je hakusema Mtumi S.A.W. katika Hadithi alioipokea Muslim (Hayatakwisha masiku na mchana paka waabudiwe Laata na Uzza)?**

Ndio, Hadithi ni swahihi lakini ina baki yake wanaificha wale wanaoitolea ushahidi wa kuwatupia Waislamu shirki ,na hili la maskitiko ni katika khiyana ya kielimu.

**Je hili laingia akilini?! na nini baki ya Hadithi?**

Kutoka kwa Aisha amesema nilimskia Mjumbe wa Allah Rehma na Amani ziwe juu yake akisema : (Hazitakwisha siku na mchana paka wataabudiwa Laata na Uzza) nikasema Ewe Mjumbe wa Allah nilikua nadhani Allah alipoteremsha: ﴿ Yeye ndie aliemtumiliza mtumilizwa wake kwa uongofu na Dini ya Haki aidhihirishe juu ya Dini zote hata wakichukia washirikina ﴾ kua hilo litatimia, akasema : (Hakika litakua hilo kwa mda anaotaka Allah, kisha Allah atatumiliza upepo mzuri uwafishe kila mwenye tembe ndogo ya Imani moyoni mwake wabakie wasiokua na kheri watarudi kwenye dini za baba zao).[4]

(1) Imepokelewa na Bukhari na Muslim.

(2) Kitabu: At-Tamhiid lima fil Muwatwa'a minal-Maani wal Asaniid Mlango wa Yaa ukurasa wa 264 .

(3) (Sura ya At-Tawba Aya 33)

(4) Imepokelewa na Muslim katika swahihi yake

Na hapa yaonesha wazi kwamba kuabudiwa kwa Laata na Uzza -yaliokua masanamu yakiabudiwa zama za jahilia- haitarudi ila baada Allah kuchukua roho za Waumini wote zama za mwisho zitakapodhihiri alama kubwa za Qiyama, na hili halijatokea zama zetu kwa kua Imani bado iko kwa fadhla za Allahalietukuka.

## ITIKADI YA KIMAKOSA JUU YA WAISLAMU


**Lakini je si watu wa Makaburi wanaotufu [Kuzunguka] Makaburi na kuyatukuza ni washirikina?**

Kitendo cha kutufu Makaburi ni haramu sio shirki, mana shirki ni pale atakapotia nia anaezunguka kumuabudu mwenye kaburi na hilo hakuna, bali yeye huwa akinuilia kujikaribisha kwa Allah kwa kutufu kaburi na hilo ni haramu mana Allah amejalia ibada ni kutufu Al-Kaaba wala sio Kaburi.



**Lakini si washirikina walikua wakisema neno hilo hilo: (Hatuwaabudu ila kwa ajili watukurubishe zaidi kwa Allah) Na wanaozunguka Makaburi wanataka kwa hilo kujikurubisha kwa Allah kama wale washirikina?**

Sivo , tafauti kati yao ni kubwa, mana washirikina wanakubali kua "Wanaabudu" Masanamu ili wawakaribishe kwaAllah, lakini wajinga kati ya Waislamu wasiojua hawana itikadi kua wanawaabudu (wenye makaburi), hivo tafauti hapa iko wazi baina haya mapote mawili. Wala kuzunguka kitu sio kukiabudu hicho kitu, mana sisi twazunguka Al-Kaaba wala kuzunguka kwetu sio kuiabudu Al-Kaaba bali ni kumuabudu Allah. vilevile wanaozunguka Makaburi hawayaabudu, lakini wanafanya kosa la uzushi wa kutufu Makaburi na Allah Alietukuka hakuwajaalia ibada ya kuyatufu kama tulivo-tangulia kusema.




**Je kuna dalili nyengine ya kutorudi kuabudiwa asiekuwa Allah Alietukuka kati ya Waislamu?**

Ndio, kuna dalili kadhaa miongoni mwazoni iliopokelewa kutoka kwa Jaabir bin Abdillah R.A. alisema: nilimskia Mtumi Rehma na Amani ziwe juu yake na Jamaa zake , akisema: (Hakika Shetwani amekata tamaa wamuabudu yeye wanaoswali (Waislamu) ndani mwa bara la warabu, lakini katika kuwagonganisha kati yao).[1]
Na iliopokelewa kutoka kwa Ibnu Masuud R.A. akisema; amesema Mjumbe wa Allah Rehma na Amani ziwe juu yake na Jamaa zake: (Hakika Ibilisi amekata tamaa waabudiwe Masanamu kwenye ardhi ya Waarabu, lakini ataridhika kwa chini ya hilo kwenu kwa munayoyadharau katika amali zenu, nayo ni madhambi makubwa).[2]

(1) Imepokelewa na Muslim katika Swahihi yake .

(2) Ameitolesha Haakim katika Mustadrak na akaiswahihisha na akamuafiki yeye Ad-Dhahabiy .




Hawa wako kwenye Upotevu na Makosa, na ametutahadharisha nao Mtumi Rehma na Amani ziwe juu yake na Jamaa zake kabla zaidi ya miaka 1400 kama yuko na sisi sasa hivi!

Kutoka kwa Hudhaifa R.A. amesema: amesema Mjumbe wa Allah Rehma na Amani ziwe juu yake na Jamaa zake : (Hakika ninacho waogopea ni mtu aliesoma Qur'aani hadi ikaonekana uzuri wake kwake, na akawa ni mategemewa kwa Uislamu, ikambadilisha vile anavotaka Allah, akaja kujivua nayo na kuitupa nyuma ya mgongo wake, na kumuendea jirani yake na panga, na kumsingizia kufanya Shirki) akasema : nikasema: Ewe Mtumi wa Allah, nani katiyao astahili shirki, aliesingiziwa ama aliesingizia? akasema: (bali aliesingizia)" [1]




Ndio na anaefanya hivo yuko kwa khatari kubwa na ni mkosa amefanya kosa kubwa na dhambi zake ni dhambi za alouwa watu wote. Amesema Allah Alietukuka: ﴿Kwa ajili ya hilo tuliwaandikia Bani Israiili kua anae uwa mtu pasina [kuliwa] mtu au kwa kufanya ufisadi katika Ardhi, basi ni kama ameuwa watu wote, na atakaehuisha basi ni kama amehuisha watu wote, na hakika wamewajilia wao Wajumbe wetu kwa dalili za wazi kisha wengi wao baada ya hayo katika Ardhi wanafanya Israfu﴾.[2]

Na Amesema Mjumbe wa Allah Rehma na Amani ziwe juu yake na Jamaa zake: ( Kumtusi Muislamu ni ufaasiq na kumpiga vita ni Ukafiri).[3]

Twamuomba Allah atuhifadhi kutokana na Dhambi kubwa ya Kuwakufurisha na kuwasingizia Waislamu Shirki, na azihifadhi damu za Waislamu , na awaongoze ndugu zetu ambao kwamba wamepotea kwa kuwakufurisha Waislamu ikawapelekea wao kukufurisha kwenye Mauwaji na Kurepua, na twamuomba Alietukuka aukomboe Umma kutokana na Fitna zilizodhihiri na zilizofichika hakika yeye ndio muhusika wa hilo na muweza hilo na yeye ndio mwenye sikitiko zaidi ya wenye sikitiko.

(1) Amepokea Ibnu Habaan (18), na Bukhari katika "At-Taarikh Al-Kabiir" (2907), na Al-Bazzaaz (2793) ,

(2) (Al-Maaida 32) .

(3) Imepokelewa na Bukhari na Muslim .

# KUAMILIANA SAWA NA MAKOSA YA WAISLAMU



**Tukikubaliana kimjadala kua maneno mlioyaeleza juu ya khatari ya kuwasingizia Waislamu shirki na nitaja yake ni swahihi, je hilo linamaanisha Wanazuoni na wahubiri wanyamazie makosa ya kisharia na Bid'aa zilizokatazwa zilizoenea ndani mwa jamii za Kiislamu?**

La Sivo , mana hapana budi Wanazuoni na Wahubiri [watekeleze] wasmame na wajib wao wa kurekibisha yanayopingana na Sharia pamoja na kuzingatia yafuatayo :

- Arekibishe kosa kwa upole na utaratibu na hunu ndio Muongozo wa Mtumi wetu Bwana Muhammad Rehma na Amani ziwe juu yake na Jamaa zake.
- Umma kwa jumla na mapote yake umeepukana na kuangukia kwenye Kufri ama Shirki kubwa, isipokua yale yalioelezwa na maneno maalumu ya Mtumi.
- Yapasa kwa anaerekibisha makosa ya wasiosoma aondowe moyoni mwake chembe yoyote ya dhana mbaya kwa Waislamu katika vitendo vyao ama itikadi zao na ajue kua kuangukia kwao katika makosa hairuhusu kuwatuhumu na ukafiri au shirki; lau sivo haitofaidisha nasaha wala haitapelekea kwenye natija inayotakikana.
- Na ni wajibu kwa Wanazuoni waheshimu "kubobea" katika Elimu za kisharia, hivo hafai Mjuzi wa Hadithi atoe Fatwa asipokua Mjuzi wa Fiqhi, na hafai anaepokea Fatwa kurukia Ijtihaad asipokua Mjuzi wa Fiqhi.
- Wahubiri wasiokua wabobea katika Fiqhi wanahitajika sana katika kuwakurubisha vijana kwa Allah, lakini wao sio watowaji Fatwa.
- Kukufurisha ni hukmu ya kisharia ya mahkamani inapaswa Muislamu mwenye hadhari na Dini yake kujihadhari kutokana na kutolijali hilo.

# MSURURU WA
# UPOTOFU NA UDANGANYIFU

Amesema Mjumbe wa Allah Rehma na Amani ziwe juu yake na jamaa zake : (wataichukua hini Elimu [Dini] Waadilifu katika kila watkaokuja, watakaoitetea kutokana na Upotofu wa Wenye kuzidisha na Udanganyifu wa Wenye kuharibu na Ufafanuzi wa Wajinga)[1]

Wamefahamu baadhi ya wenye fikra za makosa, maneno ya Allah Mtakatifu na Mtumi wake S.A.W. kwa namna hailingani na mfumo wa kielimu uliopokewa kutoka kwa waliotangulia wema, wala kuendana na makusudio na misingi mikubwa ya Ujumbe wa Mungu.

Wakazichukua kusudi baadhi ya Aya za Qur'ani Tukufu ambazo ziliteremka kwa wasiokua Waislamu wakaziteremsha kwa Waislamu, na wakachukua Aya ambazo zimekuja si kwa jumla wakazifanya ni Maagizo ya kwa jumla, na wakapotosha maana ya Maneno ya Allah na Hadithi za Mtumi wake Mtukufu kwa namna imepelekea kukita kwa ufahamu wa kimakosa sana ndani ya akili za Waislamu wasiowasomi, uliowapelekea kwenye nyendo na vitendo havina ufungamano na Dini ya Unyenyekevu ya Kiislamu.

Tutajua kupitia Msururu huu, Upotoshaji wa maana ya Maneno ya Allah na Mtumi wake, waliouangukia wenye fikra hizi za makosa, na kutilia nguvu kwao Fahamu za makosa, kiasi kilichowafanya wawe kando na Makusudio ya Allah na Mtumi wake na Ufahamu wa Wema waliotangulia .

(1) Hadithi mash'huri ameiswahihisha Ibn Abdil Bar, na amepokewa Ahmad bin Hanbal kua Amesema: hio ni Hadithi Swahihi .

SANAD
www.sanad.network
twitter: @sanadnetwork
facebook.com/sanadnetwork
youtube.com/sanadnetwork

دار الفقيه للنشر والتوزيع
DAR AL FAQIH
PUBLICATION & DISTRIBUTION